

# MONITORING LEARNER'S PROGRESS

GREDI LA 4 - MWISHO WA MUHULA WA KWANZA - 2020



## SHUGHULI ZA KISWAHILI

Jina \_\_\_\_\_

Nambari ya mwanafunzi

Jinsia                      Kiume                       Kike

Jina la kaunti \_\_\_\_\_ Nambari la kaunti

Jina la kaunti ndogo \_\_\_\_\_ Nambari la kaunti ndogo

Jina la shule \_\_\_\_\_ Nambari la shule

### VIWANGO VYA KUTATHMINI

Kuzidisha matarajio	Kufikia matarajio	Kukaribia matarajio	Mbali na matarajio

1. Jaza pengo kwa kutumia maneno uliyopewa kwenye mabano.

\_\_\_\_\_ lilikuwa linawaka mama akafua \_\_\_\_\_ na kuzianika nje ili zikauke. Tulikuwa tunacheza nje na kakangu. \_\_\_\_\_ ulivuma sana. Muda si muda \_\_\_\_\_ yalibadilika rangi na kuwa meusi. Tulikimbia kumuita mama ili aje azianue nguo kwani ilikuwa dalili ya \_\_\_\_\_ kubwa.

(mawingu, Upepeo, mvua, jua, nguo)

2. Andika sentensi tano juu ya picha hii.



- (a) \_\_\_\_\_  
(b) \_\_\_\_\_  
(c) \_\_\_\_\_  
(d) \_\_\_\_\_  
(e) \_\_\_\_\_

3. Andika sentensi hizi vizuri.

(a) aliuza maziwa, mkate na Juma  
\_\_\_\_\_

(b) ng'ombe nimdogo yule  
\_\_\_\_\_

(c) dukani mzee kalamu amenunua  
\_\_\_\_\_

(d) chai cha kikombe  
\_\_\_\_\_

(e) analia mtoto yule  
\_\_\_\_\_

4. Tenganisha silabi za maneno haya.

- (a) kitabu \_\_\_\_\_  
(b) samaki \_\_\_\_\_  
(c) kijiti \_\_\_\_\_  
(d) ubao \_\_\_\_\_  
(e) mswaki \_\_\_\_\_

5. Taja vitu ambavyo vinapatikana nyumbani.

(a) \_\_\_\_\_

(b) \_\_\_\_\_

(c) \_\_\_\_\_

(d) \_\_\_\_\_

(e) \_\_\_\_\_

6. Tumia maneno haya kutunga sentensi

(a) pia  
\_\_\_\_\_

(b) wala  
\_\_\_\_\_

(c) lakini  
\_\_\_\_\_

(d) na  
\_\_\_\_\_

(e) kwa sababu  
\_\_\_\_\_

7. Ambatanisha jina na maana yake.

Jina

(a) kuomba radhi

(b) daktari

(c) mwalimu

(d) shule

(e) mjomba

(f) paka

maana

ni mtu anayewatibu wagonjwa

ni ndugu wa kiume wa mama


ni kuomba msamaha

ni mnyama mdogo wa nyumbani

ni mahali wanafunzi husomea

ni mtu anayefunza wanafunzi

8. Andika rangi nne za bendera ya Kenya.



(a) \_\_\_\_\_

(b) \_\_\_\_\_

(c) \_\_\_\_\_

(d) \_\_\_\_\_

9. Andika wingi wa maneno haya

(a) yai \_\_\_\_\_

(b) unywele \_\_\_\_\_

(c) mkanda \_\_\_\_\_

(d) maziwa \_\_\_\_\_

(e) shule \_\_\_\_\_

10. Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Wazazi wangu ni Bwana na Bi.Juma. Baba yangu ni rubani naye mama yangu ni askari. Jumamosi ilikuwa siku ya furaha kwa familia yangu. Mjomba ambaye ni daktari alikuja kututembelea nyumbani. Alikuja na matunda na mboga nyingi ambazo alizinunua kutoka kwa muuzaji sokoni.

(a) Andika kazi za wazazi wa mwandishi; \_\_\_\_\_na  
\_\_\_\_\_

(b) Rubani hufanya kazi gani?  
\_\_\_\_\_

(c) Askari hubeba nini?  
\_\_\_\_\_

(d) Mjomba wake hufanya kazi gani?  
\_\_\_\_\_